Haitokei kuuliwa nafsi yoyote kwa dhulma isipokuwa hupata binadamu wa mwanzo fungu (la dhambi) kutoka katika damu hiyo, kwasababu yeye ndiye muanzilishi wa kwanza kuua.

Kutoka kwa Abdallah bin Mas'udi -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-Hadithi Marfu'u: "Haitokei kuuliwa nafsi yoyote kwa dhulma isipokuwa hupata binadamu wa mwanzo fungu (la dhambi) kutoka katika damu hiyo, kwasababu yeye ndiye muanzilishi wa kwanza kuua".

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhaariy na Muslim]

Inasimulia hadithi hii sababu ya kubebeshwa mmoja kati ya binadamu damu zinazofuatia ambazo zinazomwagwa baada yake, Inasemekana kuwa ni Qaabil alimuua ndugu yake Haabil kwasababu ya kumuhusudu, wao ndio muuliwa na muuwaji wa mwanzo katika watoto wa adamu; anabeba Qaabil fungu la madhambi ya damu ambazo zinazomwagwa baada yake; kwasababu yeye ndiye aliyeanzilisha kuuwa; kwasababu kila atakayefanya baada yake anaiga kwake.

http://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/3445